# UMOJA - JARIDA

UNITED NATIONS
TANZANIA

Toleo la 91
Julai - Agosti 2020

## TANZANIA YASAJILI VIZAZI VYA WATOTO MILIONI 5 KUPITIA MFUMO MPYA WA UGATUZI WA MADARAKA



Tangu Serikali, UNICEF na wadau wengine wazindue mfumo wa usajili wa vizazi katika ngazi ya chini mwaka 2013, zaidi ya watoto milioni 5 wamesajiliwa.
***Picha | UNICEF Tanzania***

## VIDOKEZO


- UNFPA yaikabidhi Serikali ya Zanzibar vifaa 300 vya PPE
- Kutomwacha yeyote nyuma katika hatua za kukabilia COVID-19: UNAIDS yatoa msaada wa vifaa kwa jamii za Zanzibar, Dar es Salaam
- UN Women yasaidia biashara zinazoendeshwa na wanawake kufufuka baada ya madhara ya COVID-19 mkoani Arusha
- ILO, Serikali na Washirika wa Kijamii waandaa mpango kazi wa kuendeleza ujuzi nchini Tanzania


Tarehe 18 Agosti, 2020 ilikuwa siku muhimu sana kwa Tanzania kwani kama nchi ilifanikiwa kufikia jumla ya watoto milioni 5 kupitia mfumo uliorahisishwa wa usajili wa vizazi. Mfumo huo ulizinduliwa mwaka 2013 na Serikali ya Tanzania kwa ushirikiano na Shirika la Kuhudumia Watoto, UNICEF; Tigo kwa ufadhili wa Serikali ya Kanada.

Mfumo huo unafanya usajili wa vizazi kufikiwa kwa urahisi na jamii nzima. Wakati ambapo hapo zamani usajili ulifanyika tu katika makao makuu ya wilaya katika kila mkoa, hivi sasa vituo vya usajili vizazi vimeanzishwa katika vituo vya afya ambavyo vinatoa pia huduama za uzazi na matunzo ya afya ya watoto, na pia katika ofisi za watendaji wa kata na yote ni kwa kuzingatia sera ya serikali ya ugatuaji madaraka kwenda ngazi za chini.

Hii ina maana kwamba wazazi wanaweza kupata vyeti vya kuzaliwa kutoka katika vituo teule vya afya au kutoka katika ofisi ya mtendaji wa kata. Mfumo huo pia unaanzisha mchakato wa 'kituo kimoja, ziara moja' na unatumia njia ya ubunifu katika ukusanyaji taarifa. Serikali imeondoa ada kwa ajili ya usajili chini ya mfumo huu na nakala ya kwanza ya cheti cha kuzaliwa inatolewa pasipo tozo yoyote. Kampuni ya simu ya Tigo Tanzania inasaidia utekelezaji wa mpango huo kupitia ubunifu kwa teknolojia ya mawasiliano,

*Inaendelea Ukurasa wa 2*

*Kutoka ukurasa wa 1*

jambo linalowezesha uingizwaji wa taarifa za usajili wa vizazi na kutumwa katika kanzidata kuu muda huohuo mtoto anapozaliwa.

Kuna hatua kubwa imepigwa katika muda mfupi kutoka watoto 400,000 mwezi Septemba, 2016 hadi kufika watoto milioni 5 hivi sasa; kutoka katika mikoa 3 hadi mikoa 18 hivi sasa, huku mradi ukiwafikia takribani asilimia 90 au zaidi katika kila mkoa ndani ya miezi mitatu au minne tangu kuzinduliwa kwake. Mpango ni kufikia mikoa yote 26 ya Tanzania bara hadi ifikapo mwaka 2022.

Kuzinduliwa kwa mfumo huu mpya kumesaidia kuongeza upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa wa jumla kwa zaidi ya wastani wa asilimia 80 katika mikoa kumi na sita kutoka msingi wa chini ya asilimia 10 wakati wa Sensa ya mwaka 2012. Data zinaonyesha pia kwamba wazazi wameokoa takribani Dola za Marekani milioni 8 (takribani Shilingi za Tanzania bilioni 20) baada ya msamaha wa ada ya usajili. Mfumo huu unatajwa kuwa miongoni mwa usanifu bora kabisa katika mfumo wa usajili unaotegemea binadamu. Ufadhili wa kifedha wa mfumo huu umeisaidia Serikali kuanzisha modeli endelevu ya usajili wa vizazi unaolenga kuwafikia zaidi ya wasichana na wavulana milioni 5 wenye umri wa chini ya miaka mitano katika mikoa 18. Fedha hizo pia zitatumika kuchukua mfumo huo na kuuanzisha katika mikoa 8 iliyobaki ya Tanzania Bara.

Mfumo mpya wa usajili wa vizazi umeondoa tofauti iliyokuwepo kati ya maeneo ya vijijini nay ale ya mijini, kuongeza ufikiwaji wa jamii zilizo pembezoni kabisa ili zisajili watoto wao, na inaendelea kukabili vikwazo vinavyohusishwa na masuala ya jinsia katika usajili wa vizazi. Mfumo huu unatatua changamoto ya msingi ya ‘upatikanaji’ na ‘unafuu wa gharama’, ambavyo vyote vilikuwa vikwazo vikuu katika mfumo wa usajili vizazi nchini Tanzania.



Mfumo wa usajili vizazi uliorahisishwa unafanya usajili wa vizazi kupatikana kwa jamii kwa urahisi. Wakati hapo kabla ilimpasa mzazi kusafiri hadi makao makuu ya wilaya katika kila mkoa, na si katika maeneo ya usajili kama hiki kilichopo katika Wilaya ya Hai, Mkoa wa Kilimanjaro, ambacho kimeanzishwa katika kituo cha afya. ***Picha | UNICEF Tanzania***

# FAO YAFADHILI UTENGENEZAJI, USAJILI WA VIUATILIFU VYA KIBIOLOJIA VYA KUKABILIANA NA VIWAVIJESHI



Watafiti na wakulima wakifanya majaribio ya Viuatilifu vya Kibiolojia vya Vuruga katika mashamba. ***Picha | FAO Tanzania***

Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) limetoa ufadhili kwa watafiti ili kutengeneza viuatilifu vya kibiolojia vitakavyosaidia kupambana na viwavi jeshi (FAW) wanaotishia usalama wa chakula na uhai nchini Tanzania.

Timu ya watafiti kutoka katika Chuo Kikuu cha Kiafrika cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela chenye makao yake makuu jijini Arusha inayooongozwa na Bi. Never Zekeya Mwambela kwa msaada wa kiufundi kutoka FAO imefanikiwa kuendesha majaribio ya uwandani na maabara ya viuatilifu hivyo vya kibiolojia. Kwa mujibu wa Bi. Mwambela, viuatilifu hivyo vinatokana na kuvu inayojulikana kitaalamu kama Aspergillus oryzae na kupewa jina la 'Vuruga' (haribu) kutokana na uwezo wake wa kupambana na viwavi jeshi.

Kiongozi wa timu ya watafiti, ambaye alianza kufanyia kazi miradi ya kudhibiti viwavi jeshi yapata miaka miwili iliyopita kama sehemu ya mafunzo yake ya Shahada ya Udaktari wa Falsafa (Uzamivu (PhD)), alianza kwa kutenganisha kuvu ya Aspergillus oryzae na kisha alitumia sindano kuidunga kwenye mabuu ya FAW katika hatua mbalimbali za ukuaji wake. Kwa njia hiyo aliweza kupata kipimo sahihi cha kutumia na kwa majaribio kadhaa yenye mafanikio uwandani katika mikoa nane tofauti nchini alipata matokeo mazuri.

Kupitia programu ya Udhibiti wa Viwavijeshi ya Global Action, FAO imebeba jukumu la kuongoza juhudi za kukabiliana na FAW. "Moja ya malengo makuu ya Global Action ni kupunguza upotevu wa mazao kwa sababu ya FAW, kitu ambacho kinaweza kufikiwa kwa ufanisi kwa kuwapatia wakulima viuatilifu vya kibiolojia vilivyo na ufanisi," anasema Bw. Baitani Mushobozi, Mtaalamu wa Kinga ya Mimea na Usimamizi Unganifu ya Wadudu Waharibifu katika ofisi za FAO nchini Tanzania.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, utafiti uliofanywa na Bi. Mwambela na timu yake uliwezeshwa kupitia Programu ya Ushirikiano wa Kiufundi ya FAO, iliyohusisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja wa Ulaya (EU) kwa kufadhili mradi wa 'Msaada kuelekea Utekelezaji wa Sera ya Kilimo katika Kanda ya SADC' (Support Towards the Operationalization of the SADC Regional Agricultural Policy).

Bw. Mushobozi anasema usajili wa viuatilifu hivyo vya kibiolojia ulipitia Kamati ya Ushauri ya Taifa ya Kinga ya Mimea, chombo kinachotoa ithibati kwa usajili wa bidhaa.

# UNFPA YAIKABIDHI SERIKALI YA ZANZIBAR VIFAA 300 VYA PPE




Baadhi ya Vifaa vya Kijikinga na Maambukizi (PPE) ambavyo vilikabidhiwa katika Serikali ya Zanzibar na UNFPA kupitia msaada kutoka Global Affairs Canada ili kuhakikisha watumishi wa afya walio mstari wa mbele wanakingwa wakati wa kutoa huduma muhimu za afya. ***Picha | UNFPA Tanzania***

Ili kuisaidia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuendelea kutoa huduma muhimu kwa uhai na taarifa pasipo kukatishakatisha za afya ya uzazi, akina mama, watoto wachanga, watoto na vijana wa balehe (RMNCAH) – na kuhakikisha kwamba wafanyakazi wa afya walio mstari wa mbele wanakingwa wakati wakitoa huduma hizi – Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Tanzania (UNFPA) limekabidhi zaidi ya seti 300 za Vifaa vya Kijikinga Dhidi ya Maambukizi (PPE).

Vifaa hivyo vyenye thamani ya Dola za Marekani $35,143 (takribani sawa na Shilingi milioni 80), vimetolewa kwa hisani ya Shirika la Global Affairs Canada kama sehemu ya GRREAT (Girls Reproductive Health, Rights and Empowerment Accelerated in Tanzania—Afya ya Uzazi ya Wasichana, Haki na Uwezeshaji Vyakolezwa Moto Tanzania) ambapo ni pamoja na barakoa za upasuaji, barakoa za N95, vifunika nyuso, miwani myeusi ya macho, kanzu za mikono mirefu, glavu za upasuaji na zisizo za upasuaji, vitakasha mikono na dawa ya maji ya kuua wadudu.

Baada ya kupokea msaada huo wa PPE, Bi. Halima Maulid, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Afya ya Zanzibar, alitoa shukrani zake kwa UNFPA kwa misaada yake mbalimbali katika mfumo wa afya visiwani, hasa katika utoaji huduma za RMNCAH. "Kwa miaka mingi mmekuwa mkitusaidia nabado mnaendelea kushirikiana nasi ili kuokoa maisha ya wanawake na watoto hapa Zanzibar," alisema.

UNFPA inashirikiana na Serikali ya Zanzibar ili kuhakikisha kwamba huduma muhimu zinaendelea hata katika nyakati hizi zenye changamoto nyingi na kwamba watumishi wa afya, ambao wanafanya kazi ya kuokoa maisha yaw engine, basi nao pia wakingwe. Wizara ya Afya itasambaza vifaa hivyo vya PPe katika vituo vyote vya Zanzibar mapema kadiri inavyowezekana kwani tayari kumejitokeza upungufu wa vifaa fulani vya PPE, zikiwemo glavu.

Licha ya msaada wa vifaa vya PPE, UNFPA pia imetoa vifaa ya Utu ili kushughulikia suala la mahitaji ya usafi na kinga kwa wanawake na wasichana walio katika karantini wakati wa mlipuko wa COVID-19, kwa uratibu uliohusisha Serikali. Vifaa hivi vinajumuisha vitu kama vile taulo za hedhi, chupi, sabuni zenye dawa, poda ya kufulia ambavyo vyote ni muhimu kwa wasichana na wanawake wapate kutunza usafi wao binafsi.

UNFPA itaendelea kusaidia juhudi za kuchochea maendeleo katika utekelezaji wa ahadi za kitaifa

***Inaendelea Ukurasa wa 5***

*Kutoka ukurasa wa 4*

na dunia katika kuimarisha matokeo bora ya afya ya mama na mtoto huko Zanzibar. UNFPA imetoa msaada wa kifedha kwa ajili ya ukarabati wa wadi ya akina mama katika Hospitali ya Kivunge, ambayo imepangwa kuzinduliwa mwezi ujao, jambo litakaloongeza upatikanaji wa huduma bora kwa wanawake waanaoishi Kaskazini mwa Kisiwa cha Unguja, Zanzibar, licha ya msaada wa kununua boti ya kusafirishia wagonjwa huko Zanzibar boti ya kwanza ya aina yake katika ukanda huu vyote vikifadhiliwa na Shirika la Global Affairs Canada.

## KUTOMWACHA YEYOTE NYUMA KATIKA HATUA ZA KUKABILIA COVID-19: UNAIDS YATOA MSAADA WA VIFAA KWA JAMII ZA ZANZIBAR, DAR ES SALAAM




Doroth Hassan, anayetoka katika TaNPUD akiwa amevaa moja ya barakoa zilizotolewa msaada na UNAIDS. ***Picha | UNAIDS, D. Msirikale***

Hivi karibuni, Serikali ya Tanzania ilitangaza kwamba janga la COVID-19 lilikuwa limekwisha, hata hivyo, utaratibu wa watu kujikinga dhidi ya virusi vya korona ingali ajenda yake kubwa. Kwa hiyo, Shirika la Umoja wa Mataifa la UKIMWI (UNAIDS) liliunda ushirika na mashrika ya kiraia ili kusaidia jamii zilizo hatarini zaidi kuzuia kuenea kwa COVID-19.

Huko Mtopepo, Zanzibar, eneo ambalo lina matatizo makubwa ya upatikanaji wa maji na usafi wa mazingira, UNAIDS inashirikiana na Chama cha Watu Wanaoishi na VVU/UKIMWI (ZAPHA+), Programu ya Kudhibiti VVU Zanzibar, Wizara ya Afya na Serikali za Mitaa ambapo hivi karibuni ilitoa msaada wa sabuni na ndoo kwa ajili ya jamii kunawa mikono, na pia iligawa barakoa za upasuaji na glavu kwa vituo vine vya afya. Jijini Dar es Salaam, kwa ushirikiano kati ya UNAIDS, Mtandao wa Watu Wanaotumia Dawa za Kulevya (Tanzania Network for People who Use Drugs (TaNPUD)) wanawake wanaotumia dawa za kulevya na famila zao walipatiwa taarifa za COVID-19, vifaa vya msingi vya usafi (ndoo, sabuni na vitakasa mikono) na mgao wa chakula kwa familia zao.

Msaada huo na vifaa utawasaidia takribani watu 5,000 kwa kuzuia kuenea kwa COVID-19 na kutabua baadhi ya athari zisizo za moja kwa moja za janga hilo, kama vile ukosefu wa kipato na uwezekano wa kuvurugika kwa huduma za afya.

"UNAIDS imebaini umuhimu wa kusaidia jamii kujikinga dhidi vya virusi vya korona, na hata kama tunajua kuwa Serikali imefanya kazi kubwa, bado tunasisitiza kwamba hatupaswi kuacha kuchukua tahadhari na kuendelea kujikinga," alisema Bi. Salma Soud Nassib, Mratibu wa Mradi wa ZAPHA+.

*Inaendelea Ukurasa wa 6*

*Kutoka ukurasa wa 5*

Kuwalenga wanawake wanaotumia dawa za kulevya, watu wanaoishi na VVU na watu walio katika makazi yasiyo rasmi ni sehemu muhimu ya lengo la UNAIDS na Umoja wa Mataifa nchini Tanania ili kutomwacha yeyote nyuma.

"Maisha yamebadilika sana kwa watu wengi. Wanawake wanalalamika kuwa wanashindwa kumudu kukidhi mahitaji ya familia zao, kwani baadhi ya kazi za muda ambazo baadhi yao walikuwa wakifanya, hazipo tena. Msaada kutoka UNAIDS utasaidia walau kaya 25 za wanawake wanaoutumia dawa za kulevya," anasema Bi. Happy Assan, Mratibu wa TaNPUD.




Maryam Charles, Mwakilishi wa Vijana wa ZAPHA+ akiwa amebeba ndoo ya kwa ajili ya kunawia mikono iliyotolewa msaada na UNAIDS kwa jamii ya Mtopepo. ***Picha | ZAPAH+, A. Mwaita.***



Kikundi cha akina mama na mratibu kutoka katika Mtandao wa Watu Wanaotumia Dawa za Kulevya Tanzania (TaNPUD). ***Picha | UNAIDS, D. Msirikale***

# “LENGO LANGU NI KUWA MFUGAJI WA KISASA WA NYUKI KASKAZINI MAGHARIBI MWA TANZANIA”



Mzinga bora wa kisasa uliotengenezwa uli katika kiwanja cha Bw. Hija ukiwa tayari kupokea nyuki. ***Picha | UN Tanzania***

Kama sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Pamoja ya Kigoma (KJP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) hivi karibni lilitoa mafunzo kwa mafundi seremala kuhusu ‘kilimo bora cha nyuki na utengenezaji mizinga ya kisasa’. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea wakulima uwezo bora zaidi kuhusu namna ya kuunganisha ufugaji nyuki na Kilimo Kinachozingatia Tabianchi na Usimamizi/ Utunzaji wa Rasilimali za Asili.

Huku akiwa amedhamiria kujifunza na kutekeleza njia bora za ufugaji nyuki, Bw. Hija Ahmad Katobagula, mkazi wa Wilaya ya Kibondo, alishiriki kikamilifu kwa kuwa miongoni mwa washiriki katika kipindi hicho cha mafunzo ya ufugaji nyuki. Baada ya kutiwa morali nay ale aliyojifunza, Bw. Ahmad aliwahamasisha washiriki wengine kutumia vema kabisa mafunzo hayo na kudhamiria kuanzisha shamba la kisasa la ufugaji nyuki mara baada ya mafunzo.

Miezi saba baadaye baada ya mafunzo, Bw. Ahmad ameanza biashara ya ufugaji nyuki huko Kibondo na sasa amefaulu kuanzisha shamba la nyuki lenye mizingia 150 ambayo imetungikwa mahali anapoweza kupata nyuki na wakati huohuo utengenezaji wa mizinga mingine 155 unaendelea. Lengo lake ni kufikia mizinga 1,000 hadi mwishoni mwa mwaka 2020. Bw. Ahmad anamiliki misitu 10 (minne iko katika Wilaya ya Kakonko na sita katika Wilaya ya Kibondo). Misitu hiyo ina miti ya asili pamoja na ile ya kupandwa na pia ana shamba la migomba, miti ya matunda na mihogo.

“Ninataka kuwa mkulima wa kupigiwa mfano ili watu waje kujifunza kwangu, nami niko tayari kuwasaidia na kuwatia moyo,” alisema.

“Ufugaji nyuki unachangia katika utunzaji wa mazingira na una matokeo mazuri sana kwa upande wa kipato na kutengeneza ajira,” alisema Bw. Ahmad. Vilevile anawahamasisha vijana kujiunga katika kilimo hicho.

Licha ya ufugaji nyuki, Hija amejenga nyumba ya nyuki ambayo hivi sasa iko katika hatua za mwisho na humo anakusudia kuweka mizinga ipatayo 1,000. Utengenezaji wa mizingia umetengeneza ajira kwa wakazi 44 wa Mkoa wa Kigoma, wakiwemo wanawake na vijana, na ilihusisha utengenezaji wa mizinga bora, kupaka rangi na utoaji chakula kwa mafundi. Baadhi ya watengeneza mizinga walipata mafunzo ya awali kupitia Programu ya KJP.

*“Ufugaji nyuki unachangia katika utunzaji wa mazingira na una matokeo mazuri sana kwa upande wa kipato na kutengeneza ajira,”*

**Bw. Ahmad,**
**Mkazi wa Kigoma alienufaika na mafunzo ya ufugaji nyuki kama sehemu ya KJP**

***Inaendelea Ukurasa wa 8***




Mzinga bora wa kisasa uliotengenezwa uli katika kiwanja cha Bw. Hija ukiwa tayari kupokea nyuki. ***Photo | UN Tanzania***



Nyumba ya nyuki na mizinga vikiwa katika matengenezo. Matengenezo hayo yanafanywa na Bw. Hija na timu yake katika Wilaya ya Kibondo, Mkoa wa Kigoma. ***Picha | UN Tanzania***

# KUMBUKUMBU ZA SIKU YA KUPINGA BIASHARA HARAMU YA USAFIRISHAJI BINADAMU (TIP) MWAKA 2020, DODOMA




Dkt. Qasim Sufi, Mkuu wa Misheni ya IOM nchini Tanzania akitoa maelezo kuhusu Siku ya Kupinga Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu Duniani. ***Picha | IOM Tanzania***

Shirika la Kimataifa la Wahamiaji (IOM), liliungana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jumuiya ya Kimataifa kufanya kumbukumbu ya Siku ya Dunia ya Kupinga Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu (TiP) huko Dodoma katikati ya mwezi Agosti.

Maadhimisho ya Siku hiyo ya TiP kupitia Mkutano wa Ngazi ya Juu jijini Dodoma ulitanguliwa na mkutano na wanahabari huko Zanzibar na majadiliano ya kitaifa kuhusu Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu huko Dar es Salaam.

Ujumbe wa Serikali katika tukio hilo uliongozwa na Waziri wa Mambo ya Ndani (MoHA), Mh. Bw. George Simbachawene, Katibu Mkuu wa MoHA na Manaibu Makatibu Wakuu pamoja na maofisa wengine wa ngazi za juu serikalini.

Katika hotuba yake, Waziri alisisitiza umuhimu wa kuwa na njia inayoratibiwa vizuri katika kupiga vita biashara hiyo haramu ya kusafirisha binadamu. Alitoa wito kwa Sekretariati kupata uhalisia wa hali ya mambo kwa kukusanya takwimu na data maalumu za TiP. Alitoa shukrani zake kwa wadau na kuwaomba kuendelea kuisaidia Serikali katika kupiga vita biashara haramu ya usafirishaji binadamu na alirudia ahadi ya Serikali na utayari wake katika kupiga vita TiP nchini kwa kunukuu kutoka katika ujumbe wa mwaka huu: "CTumedhamiria katika Juhudi Hizi—Kufana Kazi kwa Bidii Kukomesha Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu". Alitumia fursa hiyo vilevile kuishukuru Jumuiya ya Kimataifa kwa kuendelea kusaidia juhudi za Serikali katika kukomesha kabisa TiP nchini.

Dkt. Qasim Sufi, Mkuu wa Misheni ya IOM (CoM) katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwasikilisha Shirika la Kimataifa la Wahamiaji (IOM), Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN RC), Bw. Zlatan Milisic Timu ya Nchi ya Umoja wa Mataifa (UNCT) katika tukio hilo,

*Inaendelea Ukurasa wa 10*

*Kutoka ukurasa wa 9*

ambapo katika hotuba yake alishukuru ushirikiano bora uliopo kati ya IOM na Umoja wa Mataifa kwa upande mmoja na Seriakli na wadau wengine kwa upande mwingine katika kukomesha TiP nchini.

IOM inashirikiana na Serikali, UN na washirika wengine katika kuimarisha juhudi za kuwalinda watoto, kuwalinda waathirika wa biashara haramu ya usafirishaji binadamu na manusura wa vitendo vya ukatili, na mifumo inayolenga kuimarisha haki za wafanyakazi.

Jumuiya ya kimataifa, ikiwemo IOM, inachukulia Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu kama ukiukwaji wa kiwango cha juu kabisa cha haki za binadamu. Kwa hiyo, ni jambo la muhimu mno kuchukua hatua madhubuti ili kulikomesha kabisa.



Mh. George Simbachawene, Waziri wa Mambo ya Ndani akipokea zawati kutoka miongoni mwa bidhaa zilizotengenezwa na mwathirika wa Biashara Haramu ya Kusafirisha Binadamu. ***Picha | IOM Tanzania***

## ILO YASAIDIA KUIMARISHA UZUIAJI NA UTATUZI WA MIGOGORO KAZINI

Moja ya Matokeo ya Utawala ambayo Shirika la Kazi Duniani (ILO) limefaulu kuchangia ni kwa Seriakali ya Jamhuri ya Muugano wa Tanzania kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuendana na viwango vya haki vya Kimataifa na Kikanda na kutekeleza mapendekezo yanayotolewa na mifumo ya haki za binadamu, ikiwemo utolewaji wa haki kwa wanawake, watoto na makundi mengine ya wanyonge.

Kupitia Matokeo hayo, ILO ilisaidia ujenzi wa uwezo wa taasisi katika kuzuia migogoro na kutafuta suluhu—Tume ya Upatanisho na Maelewano (CMA) upande wa Tanzania Bara na Kitengo cha Kutatua Migogoro (DHU) upande wa Zanzibar. Kutokana na kujenga uwezo wa CMA na DHU, taasisi hizi ziliimarishwa ili kutatua migogoro ya kazi kwa kuendana na sheria za kazi na viwango vya kazi vya kimataifa. Programu kama hizo za ujenzi wa uwezo zilihusisha wapatanishi wa kike na kiume (45 kutoka CMA na 10 kutoka DHU) wanaohudumu katika taasisi hizi.

Upatanisho wa migogoro ya kazi umeimarisha kutokana na programu hizo za kujenga uwezo katika mbinu za upatanisho kulikofanywa kwa ajili ya wapatanishi wa CMA na DHU.

*Inaendelea Ukurasa wa 11*

*Kutoka ukurasa wa 10*

Kutokana na ujuzi wa kupatanisha kuimarika, viwango vya mafanikio katika utatuzi wa migogoro umeongezeka kote Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa mujibu wa Bw. Shanes Nungu, Mkurugenzi wa CMA, kuimarika kwa uwezo wa CMA kumewezesha kutatua migogoro ya kazi na kuvuka malengo yaliyokuwa yamewekwa na taasisi hizo.

Data zilizopo zinaonyesha kwamba katiak mwaka 2019/20, CMA ilifaulu kutatua migogoro 8,366. Lengo la mwaka huo lilikuwa kesi 3,500, jambo linaloonyesha kwamba utendaji ulikuwa wa juu sana. Mkurugenzi aliishukuru ILO na UN kwa msaada wao wa kuhakikisha kwamba migogoro ya kazi inamaamuriwa kwa wakati, na kwamba haki za wafanyakazi wanawake na wanaume zinalindwa kwa mujibu wa sheria za kazi na viwango vya kazi vya kimataifa.



Maafisa wa Tume ya Upatanisho na Maelewano (CMA) na Kitengo cha Kushughulikia Migogoro (DHU) wakishiriki katka moja ya programu za kujenga uwezo katika upatanisho na migogoro ya kazi. ***Picha | ILO Tanzania***

Msaada wa ILO pia uliopngezwa na DHU. Kwa upande wake, Bw. Modest Damian Hassan, Mkuu wa Kitengo cha DHU, alitoa shukrani zake kwa ILO kwa programu za kujenga uwezo zilizotekelezwa, ambazo kwa hakika zimeimarisha uwezo wa DHU kutatua kwa mafanikio migogoro ya kazi. Kwa mujibu wa Bw. Hassan, viwango vya mafanikio ya DHU katika kutatua migogoro hivi sasa ni asilimia 70. Takwimu zinaonyesha kwamba DHU ilifanikiwa kutatua kesi 142 katika mwaka 2019/20.



Bw. Wellington Chibebe, Mkurugenzi wa ILO Afrika Mashariki, akiwahutubia washiriki kutoka CMA na DHU katika warsha ya kujenga uwezo kuhusu upatanisho jijini Dar es Salaam. ***Picha | ILO Tanzania***

# SIKU YA MAONYESHO YA AMUA ACCELERATOR II: NA WASHINDI NI ...



Majaji walikuwa na kazi kubwa ya kuchagua washindi wanne wa tuzo za ubunifu. ***Picha | UNFPA Tanzania***

Kufika katikati ya mwezi Agosti, Awamu ya Pili ya AMUA Accelerator ilifikia ukomo wa mpango wake wa kulea kampuni zinazochipukia nchini Tanzania ambapo ilihitimishwa na Siku ya Maonyesho yaliyosubiriwa kwa bashasha ya matumizi ya mtandao kuonyesha kazi. Timu saba za vijana wabunifu walipambana, wakishindana katika kutetea suluhu, bidhaa na huduma za kidijitali, mbele ya jopo la majaji kwa matumaini ya kujinyakulia Dola $6,000 za mtaji mama na msaada zaidi wa kiufundi ili kuongeza ubora wa bidaa zao na kuzifanya endelevu na zenye gaharama nafuu katika kuleta ufumbuzi katika biashara.

Awamu ya Pili ya AMUA Accelerator ilianza na swali moja wakati wa uzinduzi mnamo mwezi Aprili, 2019: “Je, vijana wenye ulemavu wanaweza vipi kupata taarifa na huduma zinazozingatia rika za afya ya ngono na uzazi (SRH)?” Baada ya uzinduzi, mpango huo wa kuibua wavumbuzi ulisafiri nchi nzima na kukutana na zaidi ya watu milioni 1.1 wakiwemo vijana, wabunifu na wajasiriamali na kuwaalika kuibua ufumbuzi wa kibiashara ambao utakabili changamoto hii kwa baadhi ya makundi ya watu katika jamii walio pembezoni na kuachwa nyuma sana. Zaidi ya mawazo ya kibunifu 360 yaliwasilishwa mbele ya jopo la majaji ambapo mawazo 10 yalichaguliwa kwa ajili ya hatua inayofuatia ya mafunzo ya kina jijini Dar es Salaam, ambayo nayo yalichujwa hadi kubakiza saba ya mwisho kwa ajili ya kilele cha Siku ya Maonyesho.

***Inaendelea Ukurasa wa 13***

*Kutoka ukurasa wa 12*

Katika siku ya Maonyesho ya Kimtandao, na kufuatia mapambano makali kati ya timbu hizo saba, majaji walibakiwa na jukumu la kuchagua ubunifu nne—washindi?

- eAfya, ya Dar es Salaam, hawa wanatengeneza app ya simu ya mkononi inayotumia sauti ili kuwasaidia watu wenye matatizo ya kuona na kiwango cha chini cha kujua kusoma na kuandika kupata taarifa za SRH.
- Nulaif Centre, ya Kilimanjaro, wanaenesha kitovu cha jamii ambako vijana wenye ulemavu wanaweza kupata huduma na taarifa za SRH na pia kufanya shughuli za kujiingizia kipato.
- Frendlicom, ya Iringa, wanatayairisha jukwaa la mifumo ya kikompyuta ambayo mara moja itatafsiri lugha ya Kiswahili na kuwa maandishi na kinyume chke, hivyo kuwezesha mawasiliano kati ya watumishi wa afya na wateja wenye matatizo ya kusikia.
- Safe Box, pia ya Kilimanjaro, wanaunganisha huduma za SRH katika huduma za utoaji msaada kuitia kifurusih cha Mpango wa "Safe" kama vile vipindi vya darasani na mashauriano.

Awamu ya Pili ya AMUA – ambayo ni ushirka wa umma/binafsi kati ya UNFPA na Sahara Ventures, kwa msaada wa UK Aid – inaendeleza mafanikio ya Awamu ya Kwanza ya AMUA na inaendana na vipaumbele vya UNFPA Tanzania kutengeneza majukwaa yanayowapa vijana wajasiriamali nchini fursa ya kubuni na kukuza ubunifu na kuibuwa ufumbuzi wenye manufaa kwa ajili ya vijana wote kutumia vipawa vyao kikamilifu na kuendesha maisa bora yenye afya bora.




Friendlicom – moja ya ubunifu ulioibuka kidedea – wanatengeneza jukwaa la programu za kompyuta ambazo mara moja zitatafsiri lugha ya alama kwenda kwenye ujumbe wa maandishi wa Kiswahili na kinyume chake. ***Picha | UNFPA Tanzania***

# UN WOMEN YASAIDIA BIASHARA ZINAZOENDESHWA NA WANAWAKE KUFUFUKA BAADA YA MADHARA YA COVID-19 MKOANI ARUSHA




Jumla ya vyerehani 17 na simu 75 za kisasa zilikabidhiwa ili kuwasaidia wanawake ambao wanamiliki biashara katika jamii za wafugaji katika Wilaya ya Ngorongoro. ***Picha | UN Women***

Saiton Musa wa Arusha hakuweza kuficha furaha yake wakati akijaribu kuona kama cherehani alichokuwa ndiyo kwanza amekipokea kutoka UN Women kilikuwa kikifanya kazi vizuri. Cherehani hii ilikuwa ni sehemu ya msaada wa UN Women kuwasaidia wanawake vijana wanaofanya bishara ya ushonaji katika Wilaya ya Ngorongoro kufufua biashara zao zilizoathiriwa na janga la virusi vya korona.

"Nashindwa kuamini, sikutarajia msaada wa aina hii, nimefurahi sana kwamba msaada umekuja katika kipindi ambacho ninauhitaji sana," alisema Binti Musa mwenye umri wa miaka 21. Yeye ni miongoni mw wanawake vijana na wasichana waliobalehe ambao hawako shuleni 92 waliopokea vyereheani na simu za kiasasa za mkononi kutoka UN Women kwa kushirikiana na Baraza la Wanawake la Jamii ya Wachungaji.

Kupitia Mradi wa Energize unaofadhiliwa na Shirika la Misaada ya Kimataifa la Korea (KOICA), jumla ya vyerehani 17 na simu 75 za kisasa vilikabidhiwa kwa biashara zinazomilikiwa na wanawake katika jamii za wafugaji katika Wilaya ya Ngorongoro.

Juhudi hizo zitawasaidia wanufaika kujenga uhimilivu wa kiuchumi miongoni mwa wanawake wanaojishughulisha na ushonaji, kwani biashara ndogondogo na za kati ziliathiriwa vibaya kutokana na kuwa na akiba duni na mali chache. Kwa upande mwingine, simu za kisasa za mkononi zitasaidia kutumia majukwaa ya kidijitali kuimarisha tabia bora za uendeshaji biashara kupitia zana za kwenye simu na kuendesha biashara za kimtandao kwa kuwa na mbinu bora za utafutaji masoko na upelekaji wa haraka wa bidhaa kupitia mitandao.

***Inaendelea Ukurasa wa 15***

*Kutoka ukurasa wa 14*

Bi. Hodan Addou, Mwakilishi wa UN Women, alisema msaada huo kwa wanawake vijana na wasichana katika jamii ya wafugaji unachangia katika Mpango wa Taifa wa Juhudi za Tanzania Bara na Zanzibar za Kukabiliana na COVID-19 kwa kuzisaidia jamii zilizoathiriwa ili kujijenga upya. “Katika juhudi za huko Ngorongoro, mathalani, tunaishukuru KOICA kwa msaada wao uliotuwezesha kukidhi mahitaji ya wanawake na wasichana kwa wakati na kuchangia katika kufufua njia za kujikimu kwa wanawake na wasichana wa Arusha,” alisema Bi. Addou.

Alisema UN Women limeandaa vema programu zake ili kukidhi mahitaji mapya ya usawa wa jinsia na vipaumbele ili kuisaidia Serikali kujijenga upya. “Katika kazi zetu, juhudi zinazolenga usawa wa jinsia ziko ndani ya ufumbuzi wa muda mfupi na muda mrefu wa awamu za ufufuaji maisha ya kijamii, na tunafanya haya ili kujenga jamii moja yenye usawa ambayo itakuwa na uwezo mkubwa wa kuhimili mitikisiko ya siku za usoni,” alisema Bi. Addou.




Saiton Musa mwenye umri wa miaka 21 hivi sasa akipanua biashara yake ya kushona baada ya kupokea cherehani kipya kutoka katika msaada wa kufufua biashara baada ya janga la COVID-19 kutoka kwa UN Women. ***Picha | UN Women***

# MUKHTI: MJASIRIAMALI WA MIKOBA YA SHANGA



Baadhi ya mikoba ya shanga iliyotengenezwa na Mukhti ikiwa tayari kuuzwa. ***Picha* | *©UNHCR/Edward Ogolla***

"Hakuna mtu anayefanya uamuzi wa kuondoka nyumbani kwa kirahisi," anasema George Kuchio, Naibu Mwakilishi wa UNHCR nchini Tanzania akiongeza kusema kwamba "Watu wanakimbia makwao na kile tu wanachoweza kubeba mikononi mwao kwa matumaini kwamba uamuzi huo utawafikisha pahali salama kwa maisha yao."

Katika kipindi cha miaka 50 iliyopita, wakimbizi kutoka kote afrika, na je ya hapo wametafuta usalama wa maisha yao nchini Tanzania. Hivi sasa nchi hii pamekuwa nyumbani kwa takribani wakimbizi 280,000 ambao wengi wao wanaishi zaidi kwenye makambi, lakini mmoja katika wakimbizi hao saba anaishi maeneo ya mjini, miongoni mwa jamii za wenyeji. Mukhti (si jina lake halisi), mwenye umri wa miaka 41, ni miongoni mwao.

Mukhti alikimbia machafuko katika nchi yake ya asili ya Somalia mwaka 1993 na mwanzoni alipata pepo kule Zanzibar. Baada ya kutalikiwa mwaka 2009, alihangaika kuwalisha watoto wake nane, kisha alihamia Dar es Salaam ili kutafuta fursa bora zaidi. Kama walivyo wanawake wengine, Mukhti anatumia ujuzi wake wa kufuma na kushona ili kutengeneza bidaa za mikono na kujipatia fedha za ziada ili kuisaidia familia yake.

"Nililazimika kujifunza mwenyewe jinsi ya kutengeneza mikoba na kuipamba kwa shanga," anasema Mukhti. Muda mfupi baadaye, huku akipata msaada wa Dola 13 (kama Shilingi elfu 30) tu kutoka kwa majirani alianzisha biashara ndogo ya kufuma mikoba. Mukhti huuza mikoba hiyo kwa kupita nyumba hadi nyumba na kila mkoba unamwingizia kati ya Dola $2–$6 (kama Shilingi 5,000 hadi 15,000). "Biashara hii inanishughulisha na inanipauwezo wa kununua chakula zaidi na nguo kwa ajili ya familia yangu," anaongeza kusema.

Wakati ambapo wakimbizi wamejidhihirisha tena na tena kwamba wanaweza kuhimili nyakati za migogoro,

*Inaendelea Ukurasa wa 17*

*Kutoka ukurasa wa 16*

wakati wa mlipuko wa virusi vipya vya korona, "UNHCR, kwa kushirikiana na mashirika washirika, ilitoa huduma za afya na msaada wa kisaikolojia na kugawa dawa za kuua wadudu, sabuni, ndoo, barakoa na vitakasa mikono kwa kaya zote za wakimbizi wanaoishi mijini," anasema George Kuchio.



Shanga anazotumia Mukhti kupamba mikoba. ***Picha* | *©UNHCR/Edward Ogolla***

Katika safari yake ya miaka 27 nchini Tanzania, Mukhti amekabiliwa na changamoto nyingi lakini pia amepata faraja kubwa kwa ukaribu kutoka kwa marafiki na majirani zake. Kama shukrani yake kwao, "kila mapumziko ya mwisho wa juma, ninawafundisha majirani zangu namna ya kutengeneza mikoba na kujipatia fedha za ziada," anasema Mukhti.

Ingawa Mukhti amekuwa mkimbizi kwa takribani theluthi mbili ya maisha yake, ana matumaini makubwa kwamba kesho yake itakuwa bora zaidi. "Kuwa mkimbizi ni hali inayobadili maisha yako kabisa, lakini hiyo haina maana kwamba maisha yako sasa yanasimama," anasema. "Ni lazima maisha yaendelee!"

> *"Watu wanakimbia makwao na kile tu wanachoweza kubeba mikononi mwao kwa matumaini kwamba uamuzi huo utawafikisha pahali salama kwa maisha yao."*
>
> **George Kuchio, Naibu Mwakilishi wa UNHCR nchini Tanzania**

## ILO, SERIKALI NA WASHIRIKA WA KIJAMII WAANDAA MPANGO KAZI WA KUENDELEZA UJUZI NCHINI TANZANIA

Wadau muhimu katika ajenda ya Maendeleo ya Ujuzi nchini Tanzania walikutana hivi karibuni jijini Dodoma kujadilana njia bora ya kuimarisha Programu ya Taifa ya Maendeleo ya Ujuzi National Skills Development Programme (NSDP). Progamu hiyo inalenga kuleta ufumbbuzi kwa tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana nchini. Programu hiyo inafanya kazi kuimarisha uwezo wa kuajirika na mbinu za ujasiriamali miongoni mwa vijana na wakati huohuo kukuza uwezo wa biashara ndogondogo na zile za ngazi ya kati (MSEs) ili kutoa fursa mpya za ajira kwa vijana wa kike na kiume.

Miongoni mwa wadau wakuu ni Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, ajira na Watu Wenye Ulemavu), kwa kushirikaina na Shirika la Kazi Duniani (ILO). Wadau wengine ni Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Wizara ya Kilimo na Taasisi ya Utafiti na Maendeleo (REPOA).

Moja ya maeneo muhimu yaliyojadiliwa nawadau ni pamoja

*Inaendelea Ukurasa wa 18*

*Kutoka ukurasa wa 17*

na uhitaji wa kuwa na mawasiliano ya kitaasisi zaidi kati ya serikali, taasisi za elimu/mafunzo na sekta binafsi. Mkurugenzi Mtendaji wa ATE, Dkt Aggrey Mlimuka, hivi karibuni alitoa wito wa kuwepo kwa juhudi zaidi za uratibu akisema, "tunapaswa kuhakikisha kwamba sekta binafsi iko tayari na inahitaji nguvukazi ya vijana wenye ujuzi ambayo tunaiandaa, vinginevyo juhudi za kuendeleza ujuzi hazitazaa matunda."


Bw. Comoro Mwenda, Ofisa wa Programu wa ILO kwa ajili ya Mradi wa ILO wa Ujuzi akiongea katika mkutano huo uliotajwahapo juu alirejea kueleza umuhimu wa kuwa na mwitikio kwa uendelezaji ujuzi unaoratibiwa vizuri. "Uwanja wa maendeleo ya ujuzi hivi sasa una wadau wengi; jukwaa hili litaturuhusu kuamua jinsi tunavyoweza kuratibu utendaji wetu vizuri zaidi na kuunda mitandao yenye ufanisi ili kukabili fursa na changamoto za baadaye katika ulimwengu wa kazi. ILO iko tayari kushirikiana na Serikali kutafuta ufumbuzi wenye ubunifu na wenye kuleta mabadiliko siku za usoni katika uendelezaji wa ujuzi," aliongeza.

Wadau walioshiriki walibaini maeneo mengine muhimu yanayohitaji kufanyiwa kazi yakiwemo uunganishwaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika sekta zote na pia ili kuleta picha halisi ya matarajio ya ujuzi.



Kipindi cha mafunzo kuhusu programu ya Utambuzi wa Mafunzo ya Awali (Recognition of Prior learning (RPL)) kilichotolewa jijini Dar es Salaam hivi karibuni. ***Picha | ILO***

# MTANDAO WA VIJANA WANAOJITOLEA WAZINDLIWA KUENDELEZA AJENDA YA HAKI ZA WATOTO TANZANIA



Katika kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Vijana, UNICEF Tanzania ilizindua kampeni ya Mpango wa Kujitolea ulioendeshwa mubashara kupitia mtandao wa webnar na uliojikita katika kuonyesha jinsi vijana wanavyoweza kusidiwa kuwa mawakala wa mabadiliko katika jamii zao. ***Picha | UNICEF Tanzania***

Wakati dunia ilipoadhimisha Siku ya Nelso Mandela mnamo Julai 17, siku hiyo ilikuwa ya kupiga hatua kubwa kwa zaidi ya vijana 1,000 abao ni sehemu ya Mpango wa Kujitolea wa UNICEF Tanzania ambao ulizinduliwa siku hiyo. Vijana hawa wanaojitolea walichaguliwa kuendeleza ajenda ya haki za mtoto nchini na wana shauku kubwa kujitolea muda, ujuzi na rasilimali ili kujenga utetezi wa haki za watoto nchini Tanzania.

Bi. Shalini Bahuguna, Mwakilishi wa UNICEF Tanzania alifafanua wajibu wa vijana katika kuuenzi urithi wa Madiba na kujitolea kwake katika kupigania haki za watoto, "Kama watu wnaojitolea kwa ajili ya haki za watoto, ninyi ni warithi wa kweli wa urithi wa Madiba kwani vitendo vyenu kwa pamoja vina nguvu ya kuleta mabadiliko katika maisha na jamii." Aliwaasa wanaojitolea kuendeleza urithi wake huo kwa moyo wote na kusherehekea ukweli kwamba kila mmoja wetu ana nguvu ya kuleta kesho iliyo bora kupitia juhudi zetu za pamoja.

Uzinduzi huo uliofanyika kwa njia ya mtandao, uliwaleta pamoja zaidi ya watu 7,000 na ulipata ugeni wa maofisa kutoka Mpango wa Dunia wa Kujitolea (Global Volunteer Initiative), Makao Makuu ya UNICEF na vijana wawili wanaojitolea kutoka Botswana na Tanzania. Mpango huo unawashirikisha vijana ambapo vijana wanaojitolea wanashirikiana kutayarisha kampeni za vyombo vya habari kuhusu masuala muhimu ya haki za watoto na vipaumbele vyake nchini. Mpango huo pia unakazia utoaji wa mafunzo ya mara kwa mara na uongozi ili kujenga uwezo wa uongozi na ujuzi wa utetezi wa wanaojitolea kuwasaidia kuwa viongozi bora na kuchangia katika jamii zao kama waleta mabadiliko.

Kwetu, UNICEF Tanzania, huu ni ushirika wa muda mrefu wenye vijana motomoto na wenye utayari wa hali ya juu ambao watasaidia sana kutoa elimu kwa masuala ya haki za watoto kupitia kujitolea," alisema Manisha Mishra, Mkuu wa Mawasiliano, Utetezi na Ushirika wa UNICEF Tanzania.

Kefilwe Moutswi, mtu anayejitolea kutoka Botswana aliwaasa wanarika wenzake kujifunza kuwa na subira, kuwa wavubinfu na kupata manufaa yanayotokana na ujuzi waliojipatika katika mafunzo ya jumla, mafunzo kazini na yale ya vitendo. Sophia Mbeleyela, anayejitolea ambaye yuko na UNICEF Tanzania, alisema vijana wanaweza kupata uzoefu mkubwa,

*Inaendelea Ukurasa wa 20*

*Kutoka ukurasa wa 19*

kujifunza kutatua matatizo na kuleta mabadiliko katika jamii kupitia moyo wa kujitolea. Aliwaasa wenzake wanaojitolea kulenga katika mabadiliko/manufaa ambayo mpango huo utailetea jamii yetu.

Kenneth Chomba, ambaye anatoka katika Global Volunteer Initiative anasema, "Hatuwezi kuendelea na mazoea pasipo kuhusisha kundi rika linalolengwa ambalo hivi sasa ni kundi kubwa la miaka 18-24 kuwahi kuingia kwenye rekodi za historia ya dunia".

## SIKU ZIJAZO WA MAADHIMISHO YA KIMATAIFA

**Septemba 21 –** Siku ya Kimataifa ya Amani

**Septemba 24 –** Siku ya Bahari Duniani

**Septemba 26 –** Siku ya Kimataifa ya Kumaliza Kabisa Silaha za Nyuklia

**Septemba 27 –** Siku ya Utalii Duniani

**Septemba 28 –** Siku ya kimataifa ya Upatikanaji Habari kwa Wote

**Oktoba 10 –** Siku ya Afya ya Akili Duniani

**Oktoba 11 –** Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike

**Oktoba 16 –** Siku ya Chakula Duniani

**Oktoba 24 –** Siku ya Umoja wa Mataifa (UN Day)

## UMOJA WA MATAIFA IMARA KWA DUNIA ILIYO BORA ZAIDI

UNITED NATIONS
TANZANIA

**Umoja wa Mataifa Tanzania**
+255 22 219 5021
info.untz@one.un.org
Website: tanzania.un.org

This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021